JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA UCHUKUZI

MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI

# TAARIFA KWA UMMA

## HUDUMA YA USAFIRI WA DALADALA WAKATI WA MAONESHO YA SABASABA DAR ES SALAAM

Kutokana na kuwepo kwa mahitaji makubwa ya huduma ya usafiri kwenda na kutoka kwenye Maonesho ya Biashara ya Kimataifa (Sabasaba) Dar es Salaam kila mwaka, Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imetoa ruhusa kwa daladala kutoa huduma ya usafiri kutoka maeneo mbalimbali ya Jiji kuelekea viwanja vya maonesho hayo kwa masharti yafuatayo:

1. Daladala husika ni lazima iwe imesajiliwa na LATRA na iwe na leseni hai ya usafirishaji.
2. Utozaji nauli usizidi viwango vya nauli elekezi vilivyoidhinishwa na Mamlaka
3. Safari iwe **inaanzia** au **kuishia** katika njia ambayo daladala imesajiliwa na sio vinginevyo. Mfano, gari la Tegeta Nyuki kwenda Makumbusho kupitia barabara ya Bagamoyo litabeba abiria kutoka Tegeta Nyuki hadi Makumbusho na litaendelea na safari hadi Viwanja vya Sabasaba na kurudi tena hadi Makumbusho kisha kuendelea na safari hadi Tegeta Nyuki.
4. Dereva ahakikishe anafuata Sheria zote za Usalama Barabarani kama vile, kutopakia katika eneo ambalo hakuna kituo na kufuata maelekezo atakayopewa mara afikapo viwanjani ili kupunguza foleni barabarani.
5. Dereva na Kondakta wavae sare safi na nadhifu na watumie lugha nzuri kwa abiria.

Mamlaka inawaagiza kuzingatia mwongozo huu.

**Imetolewa na:**
Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini
24 Juni, 2025.